**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

**Mkuu wa TAKUKURU (M) Ruvuma,**

**S.L.P 926,**

**Simu : 255 25 2600613 Nukushi 255 25 26400663**

**Barua pepe: rbcruvuma@pccb.go.tz**

**Wavuti: www.pccb.go.tz**

**RUVUMA JULAI 16, 2020**

# TAARIFA KWA UMMA

## TAKUKURU RUVUMA YAOKOA FEDHA ZAIDI YA MILIONI 338,561,024/=

**Ndugu Wanahabari;**

TAKUKURU mkoa wa Ruvuma tumekuwa na kawaida ya kutoa taarifa ya utendaji kazi na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha kila baada ya miezi mitatu ili wananchi waweze kufahamu TAKUKURU inafanya nini. Hivyo leo tumewaita hapa ofisi za TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma ili kuwapa taarifa ya utendaji katika kipindi cha kuanzia Mwezi Aprili hadi Juni, 2020.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ni chombo kilichopewa dhamana kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11, ya mwaka2007 ya kuongoza vita dhidi ya rushwa na ufisadi nchini. Hivyo tumeendelea kutekeleza matakwa ya Sheria hiyo kupitia majukumu makuu matatu: **Kuzuia rushwa**, **Kuelimisha Umma**, **Kuchunguza tuhuma za rushwa na kushitaki watuhumiwa** wanaobainika kujihusisha na vitendo hivyo kwa mujibu wa Sheria.

Leo tunatoa taarifa inayohusu utendaji kazi kwa kipindi cha robo mwaka kupitia kwenu wanahabari ili wananchi na wadau muhimu katika mapambano dhidi ya rushwa, wafahamu katika kipindi hicho ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma imefanya nini.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2020 ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma imefanya kazi zifuatazo:

## UCHUNGUZI NA MASHITAKA:

### i. Taarifa zilizopokelewa:

Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma ilipokea jumla ya taarifa 147 kutoka kwa wananchi kupitia vyanzo mbalimbali katika kipindi hicho**.** Idara zilizolalamikiwa ni hizi zifuatazo: Ardhi 18, Tamisemi 16(Halmashauri), Serikali za mitaa na vijiji 15, Taasisi za fedha 13, Polisi 13, Vyama vya ushirika 11, Afya 10, Siasa 8, Elimu 7, Mahakama 6, Nishati na Madini 4, Biashara 5(Kampuni za udalali 2 ), Utawala 4, TARURA 2, Mifugo 2, Kilimo 2, Maliasili 1, Bima 1, Uhamiaji 1, Kampuni ya ulinzi 1, Maji 1, Usafirishaji 1, TRA 1, Binafsi 2, Ujenzi 1, mifuko ya pensheni(PSSSF) 1.

### Kesi zilizoendelea Mahakamani na Kesi mpya zilizofunguliwa:

Idadi ya kesi zilizoendelea Mahakamani ni kumi na tatu (13) ambazo washitakiwa wanatoka katika idara/sekta za: Serikali za Vijiji 4, Elimu 3, Afya 2, Mifugo na Uvuvi 1, TAMISEMI 1 na Ardhi 2. Katika kipindi hicho kesi mpya tano (5) zilifunguliwa,ambapo katika Mahakama ya wilaya ya Tunduru kesi mbili zilifunguliwa, katika mahakama ya wilaya ya Nyasa kesi mbili zilifunguliwa na kesi moja ilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Songea.

Aidha, katika kipindi hicho kesi tatu (03) zilikamilika na kutolewa uamuzi na Mahakama, ambapo kati ya hizo, kesi mbili washitakiwa walipatikana na hatia, kesi moja mshitakiwa aliachiwa huru.

### ii. Fedha zilizookolewa:

Katika kipindi cha Mwezi April hadi Juni, 2020, TAKUKURU mkoa wa Ruvuma iliokoa fedha kiasi cha jumla ya shilingi **338,561,024/=** kutokana na chunguzi mbalimbali ambazo zinaendelea.

Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi 279,187,824/= zimeokolewa kutokana na uchunguzi unaoendelea katika vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) wilayani Songea, Shilingi 10,130,000/= ziliokolewa kutokana na ufuatiliaji wa makusanyo ya fedha za vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo, Shilingi 1,194,000/= ni marejesho ya fedha zilizofanyiwa ubadhirifu kwenye serikali ya kijiji cha Makwaya (Kata ya Muhukulu Lilahi). Shilingi 1,050,000/= ni marejesho ya fedha za vyama vya ushirika Wilaya ya Namtumbo. Shilingi **36,050,000/=** ni marejesho ya fedha za Benki ya Wananchi wa Mbinga (MCB), Shilingi 2,801,200/= ni marejesho ya fedha za vyama vya ushirika Mbinga, Shilingi 7,998,000/= ni marejesho ya fedha za sekta ya Elimu, shilingi 150,000/= ni marejesho ya kampuni ya udalali,

## UZUIAJI RUSHWA

**Ndugu Wanahabari,**

TAKUKURU mkoa wa Ruvuma imefanya kazi mbili za **uchambuzi wa mifumo** wilayani Tunduru kuhusiana na uendeshaji na usimamizi wa vyama vya ushirika(AMCOS), ili kubaini mianya ya rushwa na changamoto za kiutendaji ambazo kwa namna moja au nyingine zinakwamisha kufikiwa kwa malengo ya uanzishwaji wa vyama hivyo.

**Warsha tatu** zilifanyika kwenye Wilaya za Songea na Tunduru kujadili matokeo ya utafiti mdogo kuhusu uendeshaji na usimamizi wa vyama vya msingi vya ushirika vilivyopo katika halmashauri tatu za wilaya ya Songea, na pia warsha za kujadili matokeo ya utafiti mdogo katika mfumo wa ukusanyaji mapato ya halmashauri kwa njia ya kielektoniki (POS), na katika mfumo wa manunuzi ya vifaa vya ujenzi kwenye halmashauri ya wilaya ya Tunduru

Aidha katika kipindi hicho, TAKUKURU mkoa wa Ruvuma tumefanya kazi ya **kufuatilia utekelezaji wa maazimio** yaliyowekwa na wadau katika warsha zilizofanyika kuhusu Udhibiti wa mianya ya Rushwa katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya halmashauri ya wilaya ya Tunduru kwa njia ya kielektoniki (POS), na udhibiti wa mianya ya rushwa katika mfumo wa manunuzi ya vifaa vya ujenzi katika wilaya ya Tunduru

## UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO:

Katika kipindi tajwa, TAKUKURU Mkoa wa RUVUMA imefanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo nane (08), ili kujiridhisha iwapo fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo zinatumika kadri ilivyokusudiwa na kwamba kunakuwa na thamani ya fedha.

Miradi hiyo iko katika sekta za ujenzi wa miundombinu na Afya, yenye thamani ya jumla ya shilingi **Tshs 1,804,460,900/=** (Bilioni moja, milioni mia nane na nne, laki nne elfu sitini, na mia tisa). Miradi hiyo ni mitatu(03) iliyopo wilaya ya Songea ambayo ni ujenzi wa kituo cha Afya Matimila wenye thamani ya 400,000,000/=, ujenzi wa kituo cha Afya Magagula wenye thamani ya Tshs 400,000,000/=, mradi wa matengenezo ya barabara ya kutoka Maposeni hadi Likingo unaosimamiwa na TARURA wenye thamani ya Tshs 230,024,000/=. Miradi mitatu (03) iliyopo wilaya ya Namtumbo ambayo ni mradi wa ujenzi wa kituo cha Afya Mtakanini wenye thamani ya Tshs 400,000,000/=, mradi wa matengenezo ya barabara ya kutoka Mageni hadi Rwinga unaosimamiwa na TARURA wenye thamani ya Tshs 158,197,000/=, na mradi wa matengenezo ya barabara ya kutoka Libango hadi Kiburungutu unaosimamiwa na TARURA-181,239,900/=. Miradi mitatu (02) iliyopo wilaya ya Tunduru ambayo ni mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika shule ya sekondari Mgomba wenye thamani ya Tshs 25,000,000, na ujenzi wa Hostel katika shule ya sekondari Frank Weston wenye thamani ya Tshs 10,500,000/=

Katika ukaguzi wa mradi wa matengenezo ya barabara ya Maposeni hadi Likingo, ilibainika kwamba alama za barabarani (sign boards) zilikuwa hazijawekwa ambapo zilistahili kuwekewa 6, pia kuna kipande cha kilometa 3 ambacho kilitakiwa kuwekwa kifusi lakini hakikuwekwa, mkandarasi alielekezwa kutekeleza kazi hizo. Ufuatiliaji unaendelea.

**UELIMISHAJI UMMA:**

**Ndugu wanahabari;**

Katika kuendelea kutekeleza jukumu la kushirikisha na kuelimisha jamii katika mapambano dhidi ya Rushwa, TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma katika kipindi hicho imefanya yafuatayo:- Imefanya Semina 15, Mikutano ya hadhara 13, Klabu 07 za wapinga rushwa katika shule za msingi, sekondari zimeelimishwa na kuimarishwa na Makala 6 ziliandaliwa.

**MIKAKATI YA TAKUKURU MKOA WA RUVUMA KATIKA KIPINDI CHA ROBO MWAKA ILIYOANZA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA 2020:**

Tunapoanza kipindi hiki cha robo mwaka ya Julai – Septemba 2020, TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma imejipanga kuendelea kuelimisha wananchi kupiga vita rushwa katika uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka 2020, ili wasikubali kurubuniwa kwa vitendo vya rushwa. Hiki ni kipindi cha uteuzi wa wagombea na kuanza kwa kampeni za wagombea wa vyama tofauti vya siasa. TAKUKURU imejipanga kuwaelimisha wananchi wote wa mkoa wa Ruvuma ili wafahamu uchaguzi ni nini, lengo la uchaguzi, sheria zinazoongoza uchaguzi ni zipi, umuhimu wa kupiga kura na pia wafahamu thamani ya kura yao na umuhimu wa kuchagua viongozi bora.

Tunawasihi wananchi wote wa mkoa wa Ruvuma waendelee kushirikiana na TAKUKURU ili kudhibiti rushwa katika kipindi cha uchaguzi. TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma Tumejipanga kufuatilia kwa ukaribu mienendo ya wagombea na kampeni zao na wapambe wao ili kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa.

Aidha katika kipindi hiki, TAKUKURU mkoa wa Ruvuma itaendelea kufuatilia miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa katika hatua mbalimbali ili kuhakikisha thamani ya fedha inaonekana katika miradi hiyo.

Tutaendelea kufuatilia fedha za vyama vya ushirika (AMCOS) vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) ili viongozi wote na wanachama wote waliochukua fedha za vyama wazirejeshe ziweze kunufaisha wanachama wote wanaoweka akiba katika vyama hivyo.

**HITIMISHO:**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoa wa Ruvuma inaendelea kutoa shukrani za dhati kwa wadau wote katika mkoa huu kwa ushirikiano wanaotupatia na tunaendelea kuwaasa wananchi wote wa Mkoa wa Ruvuma kuendelea kushirikiana na TAKUKURU katika mapambano haya kwa kukataa kujihusisha na vitendo vya rushwa,

kukemea vitendo vya rushwa, kutoa taarifa za vitendo vya rushwa katika ofisi za TAKUKURU zilizopo katika kila wilaya au kwa viongozi mbalimbali wa Serikali.

Mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa yatafanikiwa tu iwapo wananchi wote tutashirikiana.

**“Kupambana na Rushwa ni jukumu letu wote”**

Imetolewa na:

**OWEN JASSON**
**NAIBU MKUU WA TAKUKURU (M) RUVUMA**